THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KCPE 2012

250435

# KISWAHILI
# SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO:**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

| DAY 2 |
|---|
| Wednesday - 14/11/2012 |
| 11.00 am - 12.40 pm |

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**
**Katika kijitabu cha maswali:**

**21.** Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.
   A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo
   B. njuga, tari, kinubi, fidla
   C. harimuni, marimba, msondo, maleba
   D. siwa, zeze, upatu, nembo.

Jibu sahihi ni B

**Katika karatasi ya majibu:**

[A] [B] [C] [D] [A] [B] [C] [D] [A] ▬ [C] [D] [A] [B] [C] [D] [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

902504

© *The Kenya National Examinations Council, 2012*

**FUNGUA UKURASA**

**Maswali 1 mpaka 15.**
*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Kiswahili ni mojawapo ya lugha __1__ wazungumzaji wengi. Lugha ya Kiswahili __2__ zama za ukoloni __3__ Waafrika dhidi ya wakoloni.

Hatua ya kukifanya Kiswahili lugha rasmi nchini Kenya __4__ hadhi ya lugha husika. __5__ hapo awali, tunatarajia Kiswahili kutumiwa __6__ na Kiingereza katika shughuli za kiofisi. Hata hivyo, __7__ ; patakuwa na haja ya kutafsiriwa kwa makala mengi kwa Kiswahili.

**1.** A. yenye B. zenye C. wenye D. chenye

**2.** A. ingekuwa imetumiwa B. ilikuwa imetumiwa
C. ingekuwa ikitumiwa D. ilikuwa ikitumiwa

**3.** A. kuwatambulisha na kuwaunganisha B. kuwahamasisha na kuwalinganisha
C. kuwadumisha na kuwajenga D. kuwastawisha na kuwalenga

**4.** A. imeieneza B. imeitia fora C. imeikweza D. imeivika kilemba

**5.** A. Licha ya B. Bighairi ya C. Mbali na D. Kinyume na

**6.** A. mtawalia B. mkabala C. sadakta D. sambamba

**7.** A. hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe B. hakuna marefu yasiyokuwa na ncha
C. hakuna bamvua lisilo usubi D. hakuna kubwa lisoshindwa

Mtoto ana haki __8__ . Anastahili __9__ vizuri ili kuifaa jamii __10__ . Tabia ya mtoto __11__ na jamii, hivyo tunaweza kudai kuwa mtoto ni zao la jamii. __12__ , mtoto ana haki ya lishe bora __13__ nguvu, yaani, __14__ , na kumwezesha kujikinga na maradhi kama vile __15__ . Ugonjwa huu husababishwa na kula chakula ambacho kina upungufu wa viinilishe.

**8.** A. maradufu B. akali C. anuwai D. maridhia

**9.** A. kukidhiwa B. kutunukiwa C. kuengaengwa D. kutunzwa

**10.** A. yetu B. yake C. yangu D. yenu

**11.** A. huathirika B. huathiria C. huathiriana D. huathiriwa

**12.** A. Aidha B. Aghalabu C. Yamkini D. Pengine

**13.** A. litakaompa B. itakapompa C. litakalompa D. itakayompa

**14.** A. azma B. ilhamu C. siha D. hima

**15.** A. safura B. utapiamlo C. surua D. tetekuwanga

*Kutoka swali la **16** mpaka **30**, chagua jibu lililo sahihi.*

**16.** Maneno yafuatayo yanafuatana vipi katika kamusi?
(i) muhibu
(ii) muhtasari
(iii) muhali
(iv) muhula
A. (iii), (ii), (i), (iv)
B. (iii), (i), (ii), (iv)
C. (iv), (i), (ii), (iii)
D. (iv), (ii), (i), (iii).

**17.** Umoja wa: "Nywele zao ndefu ziliwavutia," ni:
A. Nywele yake ndefu iliwavutia.
B. Nywele zake ndefu zilimvutia.
C. Unywele wake mrefu uliwavutia.
D. Unywele wake mrefu ulimvutia.

**18.** Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I-I pekee.
A. kahawa, fedha;
B. chumvi, chupa;
C. mali, chai;
D. sukari, mvua.

**19.** Ni jibu lipi lenye maelezo sahihi?
A. Muundi ni sehemu ya mkono kuanzia begani hadi kwenye kiwiko.
B. Kitengele ni sehemu ya mwisho ya mkono yenye vidole.
C. Nyonga ni sehemu ya juu ya kiuno.
D. Paji ni sehemu ya juu ya kichwa.

**20.** Hisani ni kwa wema na kunadi ni kwa:
A. kuuza;
B. kutangaza;
C. kusambaza;
D. kuchuuza.

**21.** Chagua kinyume cha: 'Wageni waliwasili kabla ya eropleni kupaa.'
A. Wenyeji waliondoka baada ya eropleni kutua.
B. Wenyeji waliondoka kabla ya eropleni kutua.
C. Wageni waliondoka kabla ya eropleni kutua.
D. Wageni waliondoka baada ya eropleni kutua.

**22.** Tikiti, limau na fenesi ni matunda ilhali wimbi, mahindi na mtama ni:
A. miti;
B. vyakula;
C. nafaka;
D. mbegu.

**23.** $\frac{6}{9}$ kwa maneno ni:
A. sudusi sita;
B. tusui sita;
C. tusui tisa;
D. sudusi tisa.

**24.** Kukanusha kwa: "Nyungu iliyonunuliwa iliuzwa tena," ni:
A. Nyungu iliyonunuliwa haijauzwa tena.
B. Nyungu iliyonunuliwa haikuuzwa tena.
C. Nyungu isiyonunuliwa haijauzwa tena.
D. Nyungu isiyonunuliwa haikuuzwa tena.

**25.** Ni jibu lipi ambalo **si** aina ya shairi?
A. kibwagizo;
B. tathlitha;
C. ngonjera;
D. tarbia.

**26.** Onyesha sentensi yenye kielezi cha mahali.
A. Hukimbizana mara kwa mara.
B. Wanafunzi watafuzu mwakani.
C. Kambo alisafiri kwa gari.
D. Tulielekezwa pembezoni.

**27.** Kiambishi 'ka' katika sentensi: "Alienda shuleni akasome Kiswahili;" kinaonyesha:
A. kufuatana kwa matukio;
B. kulazimika;
C. kusudi;
D. kutegemeana kwa matendo.

**28.** Chagua kundi linaloonyesha kitenzi kilichoundwa kutokana na kivumishi.
A. Mvumilivu - uvumilivu;
B. Mwaminifu - aminika;
C. Mapishi - pikika;
D. Wacheshi - ucheshi.

**29.** Kitara ni upanga mwembamba wa kuongozea gwaride. Kitara vile vile ni:
A. sehemu iliyotengenezwa kukaushia mbegu;
B. chombo kitumiwacho kufungia mlango;
C. nazi changa ambayo haijawa dafu;
D. sehemu inayopandwa mimea au miche.

**30.** Chagua sentensi ambayo imetumia 'na' kama kiunganishi.
A. Wafanyakazi wote wameitwa na nokoa shambani.
B. Wafanyakazi waliokuja wanajulikana na nokoa wao.
C. Wafanyakazi na nokoa wao wanalima shamba.
D. Wafanyakazi walikuwa na matumaini ya kumwona nokoa.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Kuna aina mbili kuu za misitu. Ipo ile ya kiasili kama vile Msitu wa Karura na Msitu wa Mau. Hali kadhalika, ipo misitu ya kupandwa kama ile ya Kinale na Webuye. Misitu ni hazina kubwa kwa jamii yoyote ile. Kila mwanajamii anapaswa kujivunia misitu.

Misitu husheheni miti ya aina nyingi ambayo, pamoja na kuwa makazi ya wanyama, hutoa vyakula kama vile matunda na majani ambayo huwafaidi binadamu na viumbe wengine. Bila misitu binadamu na wanyama wangeangamia.

Misitu ni kivutio cha watalii. Watalii kutoka ndani na nje ya nchi huzuru misitu na mbuga mbalimbali za wanyama kuajabia uzuri wake. Watalii hawa hulipa fedha za kigeni ambazo hutumiwa kuanzishia miradi ya kiuchumi kama vile kustawisha miundomsingi.

Fauka ya hayo, misitu husafisha hewa na kurembesha mandhari wanamoishi binadamu. Rangi ya kijani kibichi na maua yenye rangi tofautitofauti huyafanya mazingira kupendeza hata yakitazamwa kwa mbali. Mandhari yasiyo na miti hayakosi urembo tu, bali huwa wazi kiasi kwamba hata mapaa ya majengo yaliyo hapo wakati mwingine hupeperushwa na upepo mkali.

Vipindi virefu vya jua huwanyima viumbe starehe na huweza kusababisha saratani ya ngozi kwa binadamu. Miti hufanya vivuli ambavyo huwakinga watu na wanyama dhidi ya miale ya jua. Isitoshe, si ajabu kuwa mahali ambapo pana miti mingi kwa kawaida hupata mvua hata wakati usio wa majira ya mvua kwingineko.

Sekta ya tiba imefaidika si haba kutokana na miti. Matabibu wa kienyeji na hata wa kisasa hutumia mizizi, majani na magome ya miti kutengenezea dawa. Miti kama vile mwarubaini hutibu magonjwa mengi. Hivi sasa magonjwa kama vile bolisukari, shinikizo la damu na ugonjwa wa figo **yameweza kudhibitiwa** kwa kutumia dawa zinazotokana na miti. Inasemekana kuwa hata nyoka humtibu nyoka mwenzake kwa majani!

Miti hutumiwa viwandani kutengenezea bidhaa kama vile karatasi na samani. Viwanda hivi hutoa ajira kwa maelfu ya raia, hivyo kupunguza makali ya uhaba wa nafasi za kazi nchini.

Ni wazi kuwa uhifadhi wa misitu una manufaa tumbi nzima kwa binadamu. Hata hivyo, binadamu mwenyewe ndiye anayeiangamiza misitu yenyewe. Watu wenye mate ya fisi wamekata miti kiholela kwa ajili ya kupata kuni na kuchomea makaa ya kuuza. La kusikitisha ni kwamba watu hawa **hawadiriki** kupanda miti mingine kufidia ile waliyoikata. Wengine, kwa kutojua wanajipalia makaa, hupanda miti ambayo inakausha vyanzo vya maji na kuchangia kuenea kwa kasi kwa jangwa. Hali kadhalika, wapo warina asali ambao katika juhudi zao za kurina husababisha kuteketea kwa misitu.

Kifungu cha katiba kinachohusu mazingira na mali ya asili kinasisitiza suala la uhifadhi wa mazingira. Kila mwanajamii basi ana jukumu la kuilinda misitu na kuepuka mazoea ambayo yanaiangamiza, la sivyo tutakuwa tunajichimbia kaburi.

**31.** Kulingana na kifungu, mchango wa utalii kwa jumla ni:
A. kuongeza fedha za kigeni kwenye mbuga;
B. kuboresha miundomsingi kwenye misitu;
C. kuimarisha uchumi wa nchi;
D. kuwekeza miradi ya nchi.

**32.** Chagua hasara za kutohifadhi misitu kwa mujibu wa kifungu.
A. kunyauka kwa majani, kupoteza urembo;
B. kuporomoka kwa majengo, kupoteza mvuto;
C. mahali pakavu, kuchukiza kwa mazingira;
D. upepo mkali, kunyauka kwa maua.

**33.** Ni jibu lipi sahihi kulingana na kifungu?
A. Dawa za kienyeji huponya kabisa magonjwa mengi sugu.
B. Kuhifadhi misitu kunaweza kuchangia kuongezeka kwa nafasi za kazi.
C. Mahali penye miti mingi hupata mvua inayotegemewa kila mara.
D. Kuwa na vipindi vya jua kali kunaweza kusababisha saratani.

**34.** Kifungu kinasema kuwa miti hutumiwa:
A. kutengenezea kawi na kuwasetiri viumbe;
B. kuunda samani na kuhifadhi maji;
C. kusafishia hewa na kufanikisha majengo;
D. kuvuta mvua na kuburudisha viumbe.

**35.** Maana ya methali, "**Mwiba wa kujichoma hauambiwi pole**," imedhihirika katika kifungu kwa vile:
A. Watu ndio wanaojisababishia hali mbaya ya ukame kwa kupuuza umuhimu wa miti.
B. Watu ndio wanaojisababishia hali mbaya ya kiangazi kwa kupuuza umuhimu wa misitu.
C. Watu ndio wanaojikaushia visima kwa kupanda miti isiyofaa.
D. Watu ndio wanaojichomea misitu kwa kurina pasipostahili.

**36.** Mwandishi anaonyesha kuwa kichocheo **kikuu** cha kukata miti ni:
A. kuwa na haja ya kuuza makaa;
B. kuwa na hamu ya kupata asali;
C. kuwa na tamaa ya mali;
D. kuwa na mahitaji ya kuni.

**37.** Ni jibu lipi ambalo **si sahihi** kulingana na aya ya **nane**?
A. Ukataji miti unapaswa kuandamana na upandaji miti upya.
B. Shughuli yenye faida huweza kuishia kuwa janga.
C. Ukosefu wa maarifa unaweza kusababisha hasara.
D. Jaribio la kupanda miti linastahili kuepuka panapotolewa maji.

**38.** Kulingana na aya ya mwisho:
A. Mazingira huhifadhiwa kupitia kwa kifungu cha katiba.
B. Mwanajamii hujiletea majuto kwa kutoepuka mienendo isiyokubalika.
C. Mazingira huharibiwa na hulka zisizofaa za binadamu.
D. Mwanajamii anastahili kufuata mshawasha wa katiba.

**39.** Kwa mujibu wa taarifa, '**yameweza kudhibitiwa**', ina maana:
A. Yameweza kuondolewa;
B. Yameweza kuzuiliwa;
C. Yameweza kutibiwa yote;
D. Yameweza kupunguzwa yote.

**40.** Maana ya, '**hawadiriki**', kulingana na kifungu ni:
A. hawawahi;
B. hawaambulii;
C. hawarauki;
D. hawawazii.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Tenga alilelewa katika mazingira yaliyojaa neema, furaha na uchangamfu. Wazazi wake Bwana Mtanga na Bi. Zuhura walikuwa wakwasi wa kutajika katika janibu hizo, si kwa mali tu bali kwa nyoyo zao zilizokuwa tayari kila mara kuwakirimu wanakijiji kwa lolote.

Bwana Mtanga na Bi. Zuhura hawakulala maskini wakaamka matajiri. Mtanga alianza kazi kama tarishi katika Makavazi ya Umma. Ingawa hii ilikuwa kazi ya kijungu jiko mekoni, Mtanga **hakwenda nguu**; alijitahidi kwa vyovyote vile kujinyanyua. Akajisajili kwa kozi mbalimbali za usimamizi wa makavazi na kuhitimu vyeti tofautitofauti vikiwemo stashahada na shahada katika masuala ya usimamizi wa mashirika ya umma. Jitihada zake zikazaa matunda. Akapandishwa cheo mwaka baada ya mwingine hadi akawa msimamizi wa Makavazi ya Umma. Baadaye akaajiriwa na shirika la Msalaba Mwekundu kama Mkrurugenzi wa Huduma za Kijamii.

Bi. Zuhura naye, baada ya kuhitimu masomo ya shule ya upili, alisomea taaluma ya ukutubi na baadaye kuajiriwa katika maktaba ya chuo kikuu cha Tungama. Hapa Zuhura alitambua kuwa amepata nafasi adimu ya kuutia makali ubongo wake. Akajisajili kwa kozi ya ukutubi na kuhitimu shahada ya daraja la kwanza katika taaluma hii. Wakuu wake kazini wakavutiwa na juhudi zake na kumpandisha cheo, akawa Mkutubi Mkuu.

Wakati Bwana Mtanga na Bi. Zuhura walipokuwa wakijiendeleza kitaaluma na kiuchumi, Tenga naye alikuwa anajikulia tu kama uyoga bila mpalilizi. Nyadhifa za wazazi wake zilimpokonya Tenga ushirika wa wazazi wake. Ile michezo yake na wazazi wake kabla ya chajio, yale matembezi ya kila Jumapili ... yote yakatoweka. Baba na mama wakawa wanarudi nyumbani baada ya saa nne usiku wakiwa wametoka kwenye masomo ya kuupigia msasa ujuzi wao; Jumamosi na Jumapili wana majadiliano na wanafunzi wenzao. Nyakati nyingine wazazi wote wawili walikuwa kwenye safari za kikazi. Nyakati kama hizi Tenga angepelekwa kwa shangazi ambako angekaa na kijakazi wake kwa wiki tatu; anaenda shuleni na kurudi huko huko kwa shangazi.

Wahenga walisema kwamba, akosaye la mama hata la mbwa huamwa. Pengo la malezi lililoachwa na wazazi wa Tenga lilijazwa na walezi wengine, wakiwemo vijakazi, shangazi, marika, walimu, majirani na hata vibonzo! Tenga alijifunza mengi kutokana na walezi hawa. Alifunzwa namna ya kupigana miereka, kutumia ujanja kujitoa katika matatizo, kutumia maneno makali **kujihami** alipochokozwa na wenzake, pamoja na mitindo mbalimbali ya kujinadhifisha.

Mafunzo ambayo Tenga aliyapata, hasa kutoka kwa marika, yaliutia ila mwenendo na uhusiano wake na walimu. Darasani akawa haishi kuvuruga masomo kwani kila mara angetenda kituko ili mwalimu na wanafunzi waubaini uwepo wake. Vituko hivi vilisababisha kudorora kwa alama zake. Walimu wakajaribu kuurekebisha utundu wake lakini zikawa kama juhudi za mfa-maji. **Tabia ya Tenga haikuwa ufa tena bali ukuta ambao ulihitaji kujengwa upya**. Mkuu wa Idara ya Ushauri na Uelekezaji shuleni ilibidi ahusishwe. Akamhoji Tenga na kupambaukiwa kuwa vitendo vya Tenga vilikuwa na asili ambayo ilihitaji kuchunguzwa. Akampendekezea mwalimu wa darasa kuwashirikisha wazazi katika kutafuta mbinu za kumwelekeza Tenga zaidi.

Bwana Mtanga na mkewe Zuhura walipoambiwa kuhusu hali ya Tenga walipigwa na bumbuazi. Hawakuwa wameyawazia madhara ya kutoshiriki kikamilifu katika malezi ya mtoto wao. Mwalimu aliwaambia ya kwamba nusura Tenga aingizwe na wenzake katika matumizi ya dawa za kulevya lakini akakataa na kusema kuwa hata babake hakujaribu kutumia kileo chochote. Wazazi waliona haya na kujilaumu. Hata hivyo walishukuru ya kwamba walimu waliyagundua matatizo haya kabla hayajaiangamiza familia yao.

41. Chagua jibu sahihi kwa mujibu wa kifungu. Bwana Mtanga na Bi. Zuhura:
   A. walimlea Tenga kwa kushauriana, walikuwa mashuhuri;
   B. walimlea Tenga kwa kuchangamkiana, walikuwa maarufu;
   C. waliingiliana vyema na majirani, walipenda kusaidia;
   D. waliingiliana vyema na walimu, walipenda kutoa.

42. Utajiri wa wazazi wa Tenga ulitokana na:
   A. uwajibikaji wao katika shughuli zao;
   B. kupata vyeo katika madaraja tofautitofauti;
   C. kupata shahada na stashahada mbalimbali;
   D. uwajibikaji wao katika taaluma zao.

43. Wazo **kuu** linalojitokeza katika aya ya **nne** ni kwamba:
   A. Jambo lolote likifanywa bila ushirikiano huweza kuleta madhara.
   B. Jambo lolote likifanywa bila kipimo huweza kuleta madhara.
   C. Jambo lolote likifanywa bila utulivu huweza kuleta madhara.
   D. Jambo lolote likifanywa bila mtazamo huweza kuleta madhara.

44. Kifungu kinaonyesha kuwa ukosefu wa malezi bora husababisha:
   A. kupigana miereka daima ili kupata maslahi;
   B. kudhoofika kwa maadili;
   C. kuharibu masomo darasani ili kuonekana kote;
   D. kuharibika kwa urafiki.

45. **"Tabia ya Tenga haikuwa ufa tena bali ukuta ambao ulihitaji kujengwa upya."** Ina maana:
   A. Tabia ya Tenga ilikuwa imeharibika kabisa kiasi cha kuhitaji kurekebishwa kikamilifu.
   B. Tabia ya Tenga ilikuwa imeharibika kabisa kiasi cha kuhitaji kushauriwa kikamilifu.
   C. Tabia ya Tenga ilihitaji kushughulikiwa kikamilifu.
   D. Tabia ya Tenga ilihitaji kutambuliwa kikamilifu.

46. Kwa mujibu wa kifungu, Idara ya Ushauri na Uelekezaji inasaidia katika malezi kwa:
   A. kuwahoji vijana na kuwaita wazazi wao;
   B. kutambua matatizo ya vijana na kuonyesha mbinu za kuwashirikisha;
   C. kutambua matatizo ya vijana na kuangazia mbinu za kuyasuluhisha;
   D. kuwahoji vijana na kuwaambia matatizo yao.

47. Kulingana na aya ya mwisho, wazazi wa Tenga:
   A. Hawakujua umuhimu wa kuishi karibu na mtoto wao.
   B. Walipuuza umuhimu wa ushirka wa karibu na walezi wao.
   C. Walipuuza umuhimu wa ushirika wa karibu na mtoto wao.
   D. Hawakujua umuhimu wa kuishi karibu na walezi wao.

48. Chagua jibu linaloonyesha sifa za Tenga.
   A. mcheshi, mwenye kupenda wazazi;
   B. mwenye mapenzi ya dhati, anayetafuta kushirikishwa;
   C. mchangamfu, mwenye kupenda unadhifu;
   D. mwenye msimamo imara, anayetafuta kutambuliwa.

49. Kisawe cha, '**hakwenda nguu**,' ni:
   A. hakujitia kapuni;
   B. hakujitia hamnazo;
   C. hakufa moyo;
   D. hakufa kikondoo.

50. Maana ya, '**kujihami**', kwa mujibu wa kifungu ni:
   A. kujitetea;
   B. kujinasua;
   C. kujihadhari;
   D. kujizatiti.